



ANGUKO KUBWA LA TONE



Musonda Kabwe

Edna Gicovi

Robyn Daly

ANGUKO KUBWA LA TONE

Kitabu hiki ni mali ya







bookdash.org

A TECEC project, funded by Theirworld



Anguko kubwa la Tone

(*Tone's Big Drop*)

Illustrated by Musonda Kabwe and Robyn Daly

Written by Edna Gicovi

Designed by Robyn Daly

Edited by Monique Whitaker

Translated by Aziza Abdullah Ngume

with the help of the Book Dash participants in Johannesburg on 25 February 2017.

Typeset in Barrio and Josefin Sans


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 Licence

(<http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>).

You are free to share (copy and redistribute the material in any medium or format) and adapt (remix, transform, and build upon the material) this work for any purpose, even commercially. The licensor cannot revoke these freedoms as long as you follow the following license terms:

You must give appropriate credit, provide a link to the license, and indicate if changes were made. You may do so in any reasonable manner, but not in any way that suggests the licensor endorses you or your use. No additional restrictions: You may not apply legal terms or technological measures that legally restrict others from doing anything the license permits.

ANGUKO KUBWA LA TONE




Siku moja yenye joto, Tone mdogo alikuwa
amekaa pamoja na matone mengine
angani na kutazama chini ardhini.

Ukiwa mawinguni na kutazama ardhini kila
kitu kinaonekana cha kuvutia sana.

Miti inaonekana kama mipira midogo laini
ya kijani. Mito inaonekana kama utepe wa
rangi ya fedha.

Vilele vya milima vinaonekana kama
vijiko vya barafu. Majengo yanaonekana
kama visanduku vidogo vya kijivu.









"Kuna nini kingine huko ardhini?"
Tone anamuuliza rafiki yake Nyunu.

"Baba yangu anasema kuna watu,
wanyama, miti na magari,"
Nyunu akasema.

"Huree! Kuna mambo mengi ya kuona!"
Tone akasema.

Kadri siku inavyoendelea, rafiki yao Bi.
Jua anapanda juu na juu zaidi angani
hadi Tone, Nyunyu, na matone mengine
hawawezi kumwona tena.





Bwana Upepo anakuja akipiga
mluzi wenyé ala za muziki tamu sana.

Mluzi wake unawapeperusha Tone,
Nyunyu, na marafiki zao matone kutoka
kwenye wingu lao.

“Brr!” Tone akasema.

Kunaanza kuwa na baridi kali sana.




Bwana Upepo anaendelea kupiga mluzi na
Tone, Nyunyu, na matone mengine
wanaanguka kwenye wingu lingine.

BOOP!




Wanagonga kwenye wingu kisha
wanaanguka mbali, mbali kuelekea ardhini.

"Nyonyu angalia jinsi ninavyoanguka,
Ninaenda haraka kuliko wewe!" akasema
Tone na akaanza kushindana na Nyonyu
kuona ni nani anakimbia zaidi.




Wanazidi kuanguka na kuyaacha mbali
mawingu, ndege, na majengo marefu sana.




"Tone tazama ile. Nini hiyo?" Nyunyu akasema.

Wanaenda
chini,
chini,
chini zaidi.
Kwa haraka haraka sana.




"Hmm, Ninaona nyekundu na machungwa, njano na kijani, bluu na zambarau," Tone akasema.




"Inaonekana kama mpira
mkubwa!" Nyunyu akasema.



“Unaonekana kama upinde wa mvua!”
Tone akasema.





Wakaanguka

chini,


chini,

chini.



“Whee!”

“Whee!”





Swoosh!

Wanateleza na huku wakidunda dunda
kwenye kitu kikubwa chenye rangi nyingi.

"Ni mwavuli!" Tone na Nyunyu
wanapaza sauti.



